SUMAIT University Journal (SUJ)
eissn (2953-2698)
Issue No.17 Decembre 2024

DHIMA ZA MAJINA YA PEKEE KATIKA METHALI NA MISEMO YA KISWAHILI YA ZANZIBAR

Fatma Maulid Othman
(bifatmamau@gmail.com)
Skuli ya Kiswahili na Lugha za Kigeni
Chuo Kikuu Cha Taifa la Zanzibar (SUZA)
Dkt. **Masoud Nassor Mohammed**
(masoud.mohamed@suza.ac.tz)
Skuli ya Kiswahili na Lugha za Kigeni
Chuo Kikuu Cha Taifa la Zanzibar (SUZA)
Dkt. Mahmoud Yussuf Haji
(mahmoud.yussuf@suza.ac.tz)
Skuli ya Kiswahili na Lugha za Kigeni

Received: September 2025, accepted: October 2025 Published: December 2025
© SUMAIT University Journal 2025

Abstract
This article is about the analysi of the roles of proper nouns in Kiswahili proverbs and sayings from Zanzibar. The original research that forms this article has used a descriptive approach with slightly statistical approach in collecting and analysing data. The researcher has selected a sample of the elderly to gether the information about the roles played by proverbs and selected sayings that have used proper nouns. The data were collected through interview method, where the researcher interviewed the participants using an interview guide. The results of this study shows that there are three types of roles found in proverbs and sayings that use proper nous; social roles, ideological and religious roles and ecoconomical liability. The analysis of the data of this article was guided by the talented theory of Onomastic through the onomastic approach to literary in the axis that says, "The names of the characters are used to show a certain purpose of the literary works.

Ikisiri
Makala hii inahusu uchambuzi wa dhima za majina ya pekee katika methali na misemo ya Kiswahili ya Zanzibar. Mbinu iliyotumika katika kukusanya data za utafiti huu ni usaili, ambapo mtafiti aliwasaili watoa taarifa kwa msaada wa mwongozo wa maswali ya usaili yaliyomwezesha kupata data ya utafiti. Utafiti uliozaa makala hii, imetumia mkabala wa kimaelezo na kwa kiasi kidogo umetumia mkabala wa kitakwimu katika kukusanya na kuchambua data. Mtafiti ametumia sampuli ya watoataarifa ya wazee kutafuta taarifa zinazohusu dhima zinazopatikana katika methali na misemo teule ambayo imetumia majina ya pekee. Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kuwa kuna dhima za aina tatu zinazopatikana katika methali na misemo inayotumia majina ya pekee; dhima za kijamii, dhima za kiitikadi na dini na dhima za kiuchumi. Uchambuzi wa data za makala hii imeongozwa na nadharia ya Onomastiki kupitia mkabala wa Onomastiki kifasihi katika mhimili usemao majina ya wahusika hutumika kuonesha madhumuni fulani ya kazi ya fasihi.

1.0 Utangulizi

Makala hii imefafanua kwa ufupi dhana ya methali na misemo pamoja na chimbuko lake. Lengo kuu la makala hii ni kuchambua dhima za majina ya pekee katika methali na misemo ya Kiswahili ya Zanzibar. Kabla ya kufanya hivyo, dhana muhimu za msingi zinazohusu makala hii zimechambuliwa kama sehemu ya utangulizi. Kisha mbinu na nadharia iliyotumika katika ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti huu zimeelezwa. Kimsingi majina ya pekee, ni dhana inayohusiana na taaluma ya lugha. Hata hivyo, tumeichunguza dhana hiyo kwa upande wa kifasihi ili kuona uhusiano uliopo baina ya sehemu hizo mbili. Ni wazi kuwa taaluma mbalimbali za kilugha zinaweza kuchambuliwa kwa kutumia nyenzo za kifasihi na kinyume chake. Makala hii ni mfano mmojawapo unaoakisi hali hiyo.

Maneno muhimu: Dhima za Majina, Pekee Methali Na Misemo, Zanzibar

1.1 Ufafanuzi wa Dhana za Msingi

Katika sehemu hii, dhana za msingi zinazohusu makala hii zimefafanuliwa. Lengo ni kuweka wazi kile kitakachojadiliwa hapo badaaye Dhana zilizoelezwa hapa ni tatu ambazo ni majina ya pekee, methali na misemo.

1.1.1 Majina ya Pekee

Majina ya pekee ni majina ambayo hutaja kitu kwa kutumia jina lake. Mara nyingi huanza kwa herufi kubwa. Kihore, Massamba na Msanjila, (2009) wanafafanua kuwa; Majina ya Pekee yanataja vitu, dhana na viumbe fulani maalumu. Maelezo haya yanakubaliana na Bukagile (2007) na Kihore (2009) walipofafanua kuwa, majina ya pekee hujumuisha majina maalumu ambayo yana sifa za pekee.

Kwa upande mwengine, majina ya pekee ni majina yanayotumika kutambulisha mtu, kiumbe, mahali, taasisi, jamii au kitu fulani cha kipekee na cha pekee katika kundi lake. Tofauti na majina ya kiujumla, majina ya pekee hayatumiki kwa wingi bali hutumika kwa kulenga kitu kimoja maalumu, kwa mfano Salma na Mungu. Wataalamu mbalimbali wa lughawiya hueleza kuwa jina la pekee si alama ya kimaumbile tu bali ni ishara ya kijamii, kiutamaduni na kihistoria inayobeba maana zaidi ya utambulisho. Bloomfield (1933) alisisitiza kuwa majina ya pekee huchukua nafasi ya alama za kiishara zinazowaunganisha watu na ulimwengu wao kwa ujumla.

1.1.2 Methali

Methali zinatokana na hekaya (masimulizi ya hadithi) za kufunza maadili katika jamii na zinakuwa na sifa bainifu; muundo mahsusi na hutawaliwa na matumizi ya tamathali za semi na sitiari husimuliwa kwa lengo la kuburudisha kufundisha au kuonya (Mlaga, 2017). Methali ni kipera cha semi katika fasihi simulizi kinachotokana na vyanzo vikuu vitatu; kwanza hadithi, pili maoni juu ya matukio fulani na tatu matukio ya kihistoria yanayobeba visa na mikasa vyenye mafunzo. (Okpewho, 1992).

Katika mataifa ya kiarabu methali zilikuwa ni sehemu ya utamaduni wa kifasihi wa bara arabu kwa maelfu ya miaka. Chanzo cha methali katika bara Arabu ni mifumo ya kijamii, kidini na kifasihi, ambayo imesababisha methali kuwa sehemu muhimu ya utamaduni wa Waarabu. Kwa kiasi kikubwa methali zilitumika kufunza maadili na tabia njema. Kwa upande wa barani Ulaya methali zilitokana na historia ya tamaduni za Ulaya, na zilitumika kumakinisha maadili, hekima na uzoefu wa kijamii. Methali nchini China kabla ya karne ya 19 mara nyingi zilitumia mifano ya wanyama wanaoonesha tabia za binaadamu. Methali hizo, zilisimuliwa kutoka vizazi hadi vizazi vingine (Sasaki, 2006).

Vile vile, jamii ya wazanzibari, katika pwani ya Afrika Mashariki hutumia methali za Kiswahili zaidi katika mawasiliano yao ya kila siku. Semi za Kiswahili kwa wazanzibari ni sehemu muhimu ya urithi wao wa kifasihi. Kwao methali zinatumika katika kuhamasisha, kufundisha maadili, tabia njema, na kuelekeza hali na matukio mbalimbali katika jamii ya Wazanzibari (Ghassan, 2003 & Muslim, 1950).

1.1.3 Misemo

Misemo ilitokana na mambo mawili makubwa; mafundisho ya kijamii na vita vya mashujaa. Kwa upande wa mafundisho ya kijamii misemo inahusiana na kuenea kwa Uislamu karne ya 7, ambapo ilielezea uadilifu, mafunzo ya kiutamaduni na elimu ya kijamii na kidini. (Muslim, 1950). Chimbuko la misemo katika jamii ya Wagiriki ni mifumo ya kijamii na kiutawala, ambayo yalijikita katika fasihi ya kivita, fasihi ya kimaadili, ujasiriamali na kujitolea. Misemo hiyo ilikuwa na kazi kubwa ya kuleta umoja wa jamii ya Wagiriki. Wahusika katika misemo ya Kigiriki walikuwa ni wanyama waliopachikwa tabia za watu kwa kufundisha tabia njema, uadilifu na ustahamilivu (Liddell & Scott, 2009). Misemo ya Kiswahili ilichipuka kutokana na matukio ya kila siku, tabia za watu na mazingira ya maisha ya jamii. Misemo mingi ilihusiana na majina ya watu, wanyama au maeneo maalumu yaliyojulikana kwa sifa fulani. Kwa kawaida misemo hutumia picha, ishara na tamathali (Wamitila, 2003).

2.0 Methodolojia na Nadharia

Ukusanyaji na uchambuzi wa data za makala hii ulitumia mkabala wa kitaamuli. Methali kumi na tano na misemo kumi na tano ya Kiswahili ya Zanzibar ilitumika kama sampuli ya utafiti huu. Usampulishaji wa kukusudia ulitumika kukusanya methali na misemo hiyo. Data za uwandani za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usaili. Mtafiti aliwasaili watoa taarifa kwa kutumia mwongozo wa usaili aliouandaa. Kwa kutumia mwongozo huo, taarifa zilizowezesha kupatikana dhima za majina ya pekee katika semi za kiswahili za zanzibar zilipatikana.

Kwa upande mwengine**,** utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Onomastiki ambayo msingi wake ni kuchunguza etimolojia ya majina ya watu na viumbe wengine. Pia, hushughulikia majina ya mahali (Okal 2012). Onomastiki ni sayansi maalumu inayochunguza ama kutalii majina ya viumbe (Crystal, 1987). Nadharia ya Onomastiki iliasisiwa na kamati maalumu ya wanaisimu iitwayo *Kamati ya Kitaifa ya Onomastiki*. Kamati hii ilizinduliwa katika kikao maalumu kilichofanyika nchini Ufaransa mwaka 1938.

Nadharia ya onomastiki inahusika na sanaa ya utoaji majina ya lugha yanayofungamana na tabia, itikadi, matumaini, woga na matukio katika maisha ya watu (Al-zumor, 2009). Jina la mtu au kitu linapotolewa huakisi sifa, uwezo, umbo, historia, mahala na tabia (Carlyle katika Auda, 2003). Katika mgao wa kionomastiki, jina linaweza kubeba sifa zaidi ya moja (Blanar, 1964).
Majina huwa na majukumu muhimu katika jamii. Umuhimu wake unaonekana katika kusaidia utambuzi wa mambo ya kibinafsi, rasmi, maswala ya kijamii, kiutamaduni na kiuchumi. Jambo la muhimu ni kuwa, kila jina huwa na maana iliyo na thamani yake (Koigi, 2008). Licha ya kuwa jamii mbalimbali huwa na majina yanayoonekana tofauti kimuundo, kinachodhihirika moja kwa moja ni kuwa, jamii nyingi huelekea kuwa na mielekeo inayofanana kwa namna mbalimbali ya kupata majina. Hivyo basi, uitaji majina kwa ujumla hutokana na utamaduni wa mazingira ya jamii ya lugha husika (Msanjila, Kihore & Massamba, 2009).

Nadharia ya Onomastiki ina mikabala mbalimbali kama vile Anthroponomastiki unaoshughulikia uchambuzi wa majina ya watu, Toponomastiki unaochunguza majina ya mahali kama vile kijiji, mto, milima na misitu, Onomastikifasihi unachambua majina ya wahusika katika kazi za fasihi. Ni mkabala unaochunguza majina ya wahusika katika kazi za fasihi kama vile matumizi ya riwaya tamthiliya hadithi fupi au mashairi. Pia huzingatia jinsi majina yaliyomo katika kazi za fasihi zinavyochunguza majina ya wahusika wake kwa madhumuni ya kisanaa, kifalsafa au kisiasa, Onomastikijamii. unaochunguza kwa kina sababu za jamii fulani kutumia majina fulani na namna majina yanavyoakisi mitazamo ya jamii Utafiti huu umetumia mkabala wa onomastikifasihi kukusanya na kuchambua data. onomastikifasihi ni njia ya kuchunguza matumizi ya majina katika kazi ya fasihi kwa kuzingatia maana, dhima na mchango wake katika maendeleo ya kazi za fasihi. Katika onomastikifasihi majina ya wahusika, sehemu au majina ya vitu huwa na uzito wa kimaana unaoendana na maudhui, ujumbe au dhamira kuu ya mwandishi (Mbele, 1986).

Majina ya wahusika, hutumika kama mbinu ya mtindo kwa nia ya ubunifu na ya kuvutia. Majina huashiria tabia au nafasi ya mhusika. Wahusika hupewa majina yanayoendana na tabia zao, nafasi zao katika jamii au hatima yao. Majina ya wahusika huakisi muktadha wa kijamii na kiutamaduni. Majina ambayo hutumika kuonesha mazingira, jamii au tamaduni fulani. Majina huweza kutumika kwa njia ya mafumbo, ambapo onomastikifasihi hutumia majina kama fumbo au alama ya kuwasilisha maana kubwa zaidi kuliko inayoonekana (Njogu & Chimerah 1999).
Mkabala huu una mihimili mbalimbali. Hata hivyo, katika makala hii mhimili wa kwanza unaeleza kuwa majina ya wahusika hutumika kuonesha maudhui fulani ya kazi ya fasihi umetumika ili kupata dhima zinazojitokeza katika majina ya pekee yanayotumika katika methali na misemo ya Kiswahili.

3.0 Dhima za Majina ya Pekee katika Methali na Misemo ya Kiswahili
Dhima ni nafasi, wajibu au mchango wa mhusika katika maendeleo ya kazi ya fasihi. Dhima inahusiana na kile ambacho mhusika hufanya au huwakilisha katika kazi hiyo. Kila mhusika hupewa dhima ambayo huonesha mchango wake katika muundo wa simulizi na uwasilishaji wa dhima (Wanjala, 1986). Wahusika wakiwa wamebebeshwa majina ili yawasaidie kufikisha dhima

zao kwa wepesi, baadhi ya majina wanayobebeshwa wahusika kwa ajili ya kuwasaidia kufikisha dhima kwa hadhira ni majina ya pekee. Kwa hivyo, hapa chini tunachambua dhima za majina ya pekee yanayotumika katika methali na misemo ya Kiswahili. Kama tulivyodokeza awali, data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usaili, ambapo mtafiti aliwasaili watoa taarifa wake kuhusu dhima zinazopatikana katika majina ya pekee yaliyomo katika methali na misemo iliyoteuliwa.

Baada ya uchambuzi kufanyika, mtafiti amebaini dhima za kijamii, za kiitikadi na dhima za kiuchumi katika majina ya pekee yaliyomo katika methali na misemo ya Kiswahili. Uchambuzi wa dhima hizo umeegemezwa katika mkabala wa Onomastikifasihi kupitia mhimili wake namba moja uliotaja hapo juu.

3.1 Dhima za Kijamii

Vipengele vya semi zikiwemo methali na misemo hutumika kama njia ya mawasiliano ya kijamii. Vipengele hivyo hueneza hekima, maadili na mafunzo kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Aidha vipengele hivyo vya semi hutumika kuwa nyenzo muhimu katika kufundisha maadili, kuonya, kuhimiza tabia njema na kushughulikia changamoto za kijamii. Kwa msingi huo, lengo la makala hii la kuchambua dhima za majina ya pekee katika methali na misemo ya Kiswahili zimejitokeza dhima za kijamii kama ifuatavyo;

3.1.1 Kutambulisha jamii

Sehemu hatari ni mahala au eneo lolote ambalo linaweza kusababisha madhara kwa watu au kwa viumbe wengine kama wanyama na wadudu endapo tahadhari hazitachukuliwa kuepukana na madhara yanayoweza kujitokeza. Sehemu hatari inaweza kuwa: baharini, mtoni, kiwandani, sehemu za ujenzi au katika utumiaji wa vifaa kama shoka. Kwa namna ambayo nadharia ya onomastiki katika mkabala wa onomastikifasihi kupitia mhimili unaoitaka kazi ya fasihi kutumia majina ya wahusika kwa kulenga madhumuni maalunu, wasanifu wa methali na misemo ya Kiswahili wamekuwa wakitumia majina ya pekee katika usanifu wa kazi hizo kwa makusudio mahsusi. Mfano kutumika jina la **Pate** katika msemo usemao, *"Mwenda **Pate** harudi kirudicho ni kilio"*
Methali hii inamaana ya kwamba, mtu anayekwenda mahali pa hatari au pabaya mara nyingi hawezi kurudi salama. Badala yake hurudi na majonzi au huzuni kwa sababu ya maafa yatakayomsibu. Methali hii inawaonya watu kutokufanya maamuzi kiholela. Inasisitiza kuwa maamuzi mabaya yanasababisha matokeo yasiyotarajiwa na kuwakumbusha watu kuepuka tamaa na ushindani usio wa lazima. Kupitia methali hii, watoa taarifa wameeleza kuwa, jina la Pate limetumika kwasababu ya hatari inayotokezea mara kwa mara katika sehemu hiyo wakati wa vita baina ya jamii mbalimbali kabla ya uhuru. Mji wa Pate una historia ndefu na ya kusisimua sana. Historia inaeleza kuwa wakati fulani mji huo uliingia vitani na miji mingine mbalimbali ya mwambao wa Kenya. Hata hivyo, mara zote mji huo ulikuwa unaibuka mshindi kila unapokabiliana na mahasimu wake. Hii ndio sababu ya kupatikana kwa methali hii ya mwenda Pate harudi kirudicho ni kilio. Jamii hiyo ya Pate ikawa ni sehemu hatari sana kwa kupoteza maisha ya watu. Hivyo semi za Kiswahili zinachukua nafasi ya kutahadharisha jamii ili kuwaepusha na maafa yanayoweza kuwapata.

3.1.2 Kuepuka dharau

Dharau ni tabia ya kutothamini au kutoheshimu mtu au kitu (TUKI, 1988). Mara nyingi tabia ya dharau hufanywa na mtu anayehisi yeye ana kitu bora kuliko mwenzake, jambo hili husababisha kudharauliana miongoni mwa wanajamii. Watoa taariwa wameeleza kuwa mara nyingi mwenye utajiri humdharau masikini, mwenye elimu humdharau mjinga na vijana huwadharau wazee kwa sababu ya ujana wao. Mhimili wa mkabala wa Onomastiki kifasihi unaotambua kuwa majina katika kazi ya fasihi hutumiwa kwa makusudio maalumu, unatuongoza kutambulisha jina la pekee la "Fundi Mwalimu" lilivyotumika katika methali na kuwa na dhima ya kutaka kuepusha dharau kupitia methali isemayo:

"*Kikitengenea cha **Bwana Saidi**, kikiharibika cha **Fundi Mwalimu**"*

Jina la pekee; **Fundi Mwalimu** linakusudiwa ni mtu aliyedharauliwa na hawezi kusimamia jambo likafanikiwa. Aidha watoa taarifa wameeleza kuwa katika msemo usemao:

*"Ukila ule na **Makame** akiulizwa aungame"*

Jina **Makame** limetumika kuwa ni mtu mwenye cheo cha chini, lakini katika mamlaka ya majukumu yake haifai kudharauliwa kwa sababu ya udhaifu wa cheo alichopewa. Hivyo jamii inatakiwa ajiepushe na dharau kwani kila mmoja anaweza kusimamia au kufanya jambo lenye manufaa kwa mtu mmoja mmoja na jamii kwa jumla.

3.1.3 Utambulisho wa Miji ya Kihistoria

Mji wa kihistoria ni mji ambao una umuhimu wa kipekee kutokana na historia yake ya kijami, kiutamaduni, kisiasa, kiuchumi na kisanii. Kwa kawaida miji ya kihistoria huhifadhi mabaki ya kihistoria, michoro ya zamani au miundombinu ya kipekee. Miji hii huwa na ukongwe mkubwa na mchanganyiko wa watu wa makabila na shughuli mbalimbali, zikiwemo za kiuchumi na kijamii (Trigger, 1972)

Kwa ujumla utafiti unaeleza kuwa; miji ya kihistoria ni miji ambayo ina urahisi wa kutambulika kutokana na umuhimu wake wa kihistoria na kiasili. Hasa kwa namna inavyohifadhi urithi wake unaohusiana na biashara, dini na maisha ya jamii ya watu wake. Mji wa kihistoria si lazima uwe mkubwa sana bali ni eneo lenye kazi maalumu kwa nyakati maalumu, kama makao makuu ya biashara au dini. Mfano Mji Mkongwe wa Zanzibar ambao umejumuisha miji midogomidogo; ikiwemo Kiponda, Hurumzi, Forodhani na Vuga.

Watoa taarifa walipotoa hoja hii wameeleza kuwa Mji wa Kiponda ni mfano hai wa kihistoria ambao umezungumzwa katika methali inayoeleza kuwa;

*"Nakuona u Muunguja umekunywa maji ya **Kiponda**"*

Kiponda ni jina limetumika kwa madhumuni ya kuwakilisha miji ya kihistoria inayopatikana katika kisiwa cha Unguja. Ukiuangalia mji wa Kiponda ni miongoni mwa miji midogo inayopatikana katika Mji Mkongwe wa Zanzibar. Mji huu unafahamika vyema kihistoria si Afrika bali hata duniani kwa jumla. Pia katika msemo usemao:

"Kahamia Kianga Mselemu"

Watoa taarifa wameeleza kuwa neno **Kianga** ni jina la kihistoria linalojuilisha mji maarufu uliosifika kwa uzalishaji wa nazi na mpunga. Mji ambao watu walikuwa wakitoka katika miji yao

na kuhamia Kianga kwa ajili ya kufanya shughuli za kulima wa mpunga na ukwezi wa minazi. Melezo ya watoa taarifa yameakisa vyema mhimili wa mkabala wa Onomastikifasihi kutoka katika Nadharia ya Onomastiki unaeleza kuwa; majina yanayotumika katika kazi ya fasihi yanatumika kwa makusudio maalumu, na kwamba katika methali hii, jina la *Kiponda* limetumika kuwa ni utambulisho wa miji ya Kihistoria inayopatikana katika kisiwa cha Unguja.

3.1.4 Kuvienzi vipawa

Kipawa ni kipaji au uwezo au karama za kiroho anazopewa mtu kutoka kwa Mungu kwa ajili ya kumtumikia yeye (Dira.elimu.tz). Kipawa kinamtofautisha mtu mmoja na mwengine. Mtu mwenye kipawa anakuwa na umahasusi wake katika imani na matendo ya kiroho juu ya Muumba wake. Kwa ujumla vipawa ni uwezo au akili ya kipekee ambayo mtu hupewa kimaumbile au kinasaba, inayomuwezesha kufanya mambo kwa urahisi, ustadi au kwa ubunifu mkubwa kuliko kawaida. Vipawa hujitokeza katika nyanja tafauti anazozitumia mtu katika maisha yake zikiwemo; kipawa cha lugha, kipawa cha muziki, kipawa cha mantiki, kipawa cha michezo na kipawa cha kijamii.

Watoa taarifa wameeleza kuwa katika msemo wa Kiswahili usemao:

“Nabii hakubaliki kwao”

Neno ***nabii*** linawakilisha kipawa maalunu ambacho anakuwanacho mtu. Ingawa mara nyingi kipawa hicho huonekana ni kawaida tu kwa jamii inayomzunguuka. Maelezo ya watoa taarifa yanashabihiana na mtazamo wa Nadharia ya Onomastiki kupitia mkabala wa Onomastikifasihi kama inavyoeleza katika mhimili wake usemao katika kazi ya fasihi majina hutumiwa kwa makusudio maalumu. Hivyo basi neno nabii katika msemo huo limekusudiwa kuitanabahisha jamii kuona umuhimu wa kuwa na watu wenye vipaji na kuvienzi vipaji. Aidha kuvienzi vipaji hivyo kwa ajili ya maendeleo yao. Vipawa humwezesha mtu kurahisisha maisha yake kwa mujibu wa kipawa alihotunukiwa mtu huyo.

3.1.5 Kusisitiza uadilifu

Uadilifu ni hali kutenda haki bila ya kupendelea upande wowote (TUKI, 1988). Uadilifu ndio msingi wa kupatikana kwa haki za binaadamu. Kama ambavyo Nadharia ya Onomastiki kupitia mkabala wake wa Onomastikifasihi inaamini kuwa majina katika kazi ya fasihi hutumiwa kwa makusudio maalumu, watoa taarifa wanaeleza kuwa, msemo;

“Mungu si Athumani”

Jina la **Mungu** limetumiwa kwa madhumuni ya kubainisha kuwa Mungu siku zote ni mwenye kufanya haki kwa wanadamu, na kwamba tafauti na mwanadamu kuwa huacha kumtendea haki mwanadamu mwenzake kwa sababu moja ama nyengine, hivyo kamwe Mungu hawezi kunasibishwa na Athumani. Wala mzee mkumba, watoa taarifa wengine wamenasibisha msemo huu na ule wa Mungu si mzee mkumba wala Mungu si mfaki. Watoa taarifa wamesisitiza kuwa, uadilifu ni kwa Mumba pekee. Vilevile katika methali isemayo

“Mkataa ya Mussa hupata ya Firauna”

Imeelezwa kuwa jina la **Mussa** limetumika kuwa ni kielelezo cha mtu Muadilifu, mwenye kusimamia haki kwa mwenye haki na kueleza ukweli. Kwa hivyo, jina la Mungu limetumiwa ili

kuwataka wanadamu siku zote wajilazimishe kutenda haki kwa mwenye haki. Hata maandiko yanasema “mpe haki kila anayestahiki kupewa haki’’

3.1.6 Kuwa na matumaini

Matumaini ni hali ya kiakili au kihisia ambayo mtu anaamini au anatarajia kwamba mambo yatakuwa mazuri au yatakwenda kama alivyotarajia hata kama kuna changamoto. Mtu mwenye matumaini anakuwa na sifa zinazompambanua na mtu mwengine; anakuwa na mtazamo chanya, hujiwekea malengo, anakuwa mwenye subira, kuendelea kujaribu, huona fursa badala ya vikwazo na huwashawishi watu wengine kufanya analolitarajia (Synder, 1991).

Kwa ujumla matumaini ni hali ya kuwa na imani au matarajio juu ya jambo jema. Hii ni nguvu ya ndani inayomfanya mtu aendelee kuamini hata pale hali inapobadilika na kuwa mbaya hakati tamaa. Katika methali nyengine:

“Mwaka ni mmoja leo ***Jua*** *kesho mvua”*

Watoa taarifa wameeleza kuwa, neno *jua* limetumika katika methali hii kwa ajili ya kuonesha matumaini anayotakiwa kuwa nayo kila mtu juu ya kufikia malengo ya maisha anayoyatarajia pamoja na changamoto za hapa na pale. Nadharia ya Onomastiki kupitia mkabala wake wa Onomastikifasihi imekuja kuunga mkono maelezo ya watoataariwa kuwa, majina katika kazi za fasihi hutumiwa kwa makusudio maalumu kama ambavyo **Jua** lilivyotumika kuwa ni kitu kinachowakilisha matumaini katika methali hii. Kwa mnasaba huo, jamii inapaswa kuwa na matumaini na kuacha tabia ya kukata tamaa, kwani kukata tamaa kunasababisha kutofikia malengo ya maisha.

3.1.7 Kukataa kumkweza mgeni

Mgeni ni mtu asiye mwenyeji katika mahali au katika mji, si mkaazi wa mji huo. Amefika kwa mara ya kwanza au kwa muda mfupi. Mtu mgeni anakuwa si mkaazi wa kudumu, hajafahamika sana. Anapokelewa au kuandaliwa, anahitaji msaada wa kila jambo linalohusu jamii husika. Mara nyengine huleta mabadiliko au taarifa mpya kutoka sehemu za mbali. (BAKITA 2015 & TUKI 2015).

Kiujumla mgeni ni mtu aliyeingia katika kijiji, mji au nchi kutoka sehemu nyengine lakini si mzaliwa wala mkaazi wa sehemu hiyo. Kama ambavyo Nadharia ya Onomastiki kupitia mkabala wa Onomastikifasihi inaeleza katika mhimili wake kuwa, katika kazi za fasihi majina yanayotumiwa yanakuwa na makusudio maalumu, ndio maana Waswahili husema “mgeni hachomi nguru akanuka”. Angalia methali ifuatayo:

“Pemba peremba ukija na joho utarudi na kilemba”

Neno **Pemba** ni jina lililotumika kwa makusudio ya kumpa heshima mwenyeji wa kisiwa cha Pemba mbele ya mgeni wa kisiwa hicho. Pia lina lengo la kutanabahisha kuwa ukienda Pemba unatakiwa kuheshimu na kutii taratibu zilizowekwa vyenginevyo utadhalilika na kupoteza mwelekeo wa safari yako. Hutofikia lengo la kwenda Pemba na utarudi huna kitu bila kujali kama wewe ni mgeni.

3.2 Dhima za kiitikadi

Katika kipengele hiki, tunashughulikia zaidi itikadi za kidini. Dini ni mfumo wa maisha na desturi ambazo zinahusiana na vitu vitakatifu yaani vitu vinavyotengwa na kuheshimiwa, dini huunganisha jamii kwa kuhimiza mshikamano wa kijamii (Durkheim, 1912). Mtazamo wa dini umekuwa ukitofautiana kulingana na dini husika. Wanadamu wamekuwa wakiabudu kupitia dini tafauti zikiwepo uislamu, ukristo, uyahudi, umajusi na utawa. Kwa kuwa methali na misemo ya Kiswahili ni zao la jamii ya Waswahili, mtafiti katika utafiti huu amebaini kuwa methali na misemo yenye majina ya pekee imebeba dhima mbalimbali za kidini na itikadi, miongoni mwa dhima hizo ni:

3.2.1 Kusisitiza busara na maadili

Busara ni uwezo wa mtu kupatia ufumbuzi wa jambo kwa njia ya hekima (BAKIZA, 2010). Busara ni jambo linalohitajika katika kila jamii kwa ajili ya kusimamisha na kutatua matatizo yanayokabili kwa njia ya amani, hakuna jamii isiyohitaji busara. Watoa taarifa wa utafiti huu wameeleza kuwa, kila wakati mwanadamu anahitajika kusimamia busara na kufuata maadili. Maadili ni nguzo ya msingi katika kuimarisha imani miongoni mwa wanajamii, kupeana matumaini na faraja, ulinzi baina yao, heshima na kupeana moyo katika mafanikio chanya. Pia wanaeleza miongoni mwa methali inayosisitiza busara na maadili ni;

*"Mfuata **Mmanga** hunukia"*

Limetumika jina la *Mmanga* kuashiria utumiaji wa hekima na busara, na kwamba mtu atakayetumia busara katika utatuaji wa mambo yake atafanikiwa. Nadharia ya Onomastiki kupitia mkabala wa Onomastikifasihi unaoeleza kuwa, majina yanayotumiwa katika kazi za fasihi yanakuwa na madhumuni maalumu, ndio maana jina; *mmanga* katika methali hii limekusudiwa busara na hekima.

3.2.2 Kuonesha furaha ya pamoja

Furaha ni hali ya moyo wa mtu kuwa na shangwe, amani na utulivu kutokana na kifikiwa na jambo zuri linalopendeza kwake na kumfanya akaridhika (TUKI,1988). Jambo hilo linasimama nafasi ya hisia ya kutosheka kutokana na faraja au furaha aliyonayo mtu. Nadharia ya Onomastiki inaeleza katika mkabala wa Onomastikifasihi kuwa majina yanayotumiwa katika kazi ya fasihi yana makusudio maalumu, katika kuthibitisha mtazamo huu, watoa taarifa wameeleza kuwa: katika methali isemayo:

*"Mkaidi hafaidi mpaka **Siku ya Iddi"***

Walipotumia neno *siku ya iddi* walikuwa na makusudio maalumu, ambayo ni kuonesha ushirikiano wa pamoja wa wanajamii katika masuala yao ya kidini. Jambo ambalo linakuwa ndio msingi na chanzo cha maendeleo endelevu ya masuala ya kidini na kijamii. Kwamba mwanajamii Fulani anaposhauriwa na wenzake kuhusu jambo fulani akapuuza ushauri huo asubiri madhara yake katika siku za badaaye Inasisitiza mashauriano na maisha ya pamoja ili kudumisha furaha na maendeleo ya jamii.

3.2.3 Nafasi ya mwanadamu kwa Muumba

Mwanadamu ni kiumbe mwenye sifa za pekee tofauti na viumbe wengine Hata hivyo, yeye ana upekee katika maumbile yake. Anasimama wima na kutumia mikono kwa kazi. Mwanadamu ana akili ya hali ya juu inayomwezesha kufikiri na kutatua matatizo pamoja na kuwa na hisia kama

furaha, huzuni, upendo na hasira. Watoa taarifa wa utafiti wameeleza kuwa kutumika kwa jina la Athumani katika methali isemayo:

*Mungu si **Athumani***

Maelezo ya watoa taarifa yanaonesha kuwa, jina "**Athumani"** katika methali hii linakusudiwa kuonesha nafasi aliyonayo mwanadamu mbele ya Mungu. Kwamba uwezo na mamlaka aliyonayo Mungu hayawezi kulinganisha na ujuzi alionao mwanadamu kwa sababu Mungu ana uwezo wa kufanya Atakacho wakati wowote. Hata msemo usemao "Asiye mtu ana Mungu" nao unaonesha namna nguvu za Mungu za kuweza kumsaidia mtu anayeonekana kukosa msaada kwa wenzake, walisisitiza watoa taarifa. Dhima hiyo iliyoelezwa na watoa taarifa inaungwa mkono na Nadharia ya Onomastiki kupitia mkabala wake wa Onomastikifasihi, pale unapoeleza kuwa majina yanayotumika katika kazi za fasihi yanakuwa na makusudio yake maalumu.

3.3 Dhima za Kiuchumi

Uchumi ni taaluma ya kibiashara inayochunguza jinsi watu binafsi, makampuni na Serikali wanavyokusanya na kutumia rasilimali kwa ajili ya mahitaji yao ya kila siku katika maisha. Rasilimali hizo ni kama vile, ardhi, kazi, mtaji na ujasiriamali. (Robbins, 1932). Mtafiti amebaini kuwa katika methali na misemo ya Kiswahili inayotumia majina ya pekee kunajitokeza dhima mbalimbali za kiuchumi, miongoni mwa dhima hizo ni:

3.3.1 Kushajihisha kazi

Kazi ni mchakato wa binadamu wa kujituma ili kugeuza mazingira ya asili kuwa vitu vya matumizi kupitia juhudi zake. Kazi pia ni wito wa kiroho ambapo mtu hufanya kazi kwa bidii siyo tu kwa kipato bali kutimiza wajibu wa kiroho (Webar, 1920). Uwajibikaji ni uwezo wa mtu wa kutoa huduma kwa wengine kwa njia ya kujitolea na kuwa tayari kuwajibika kwa matokeo ya matendo au kauli zake katika majukumu anayosimamia. (Bryson, 2004).

Kwa ujumla kazi zinahitaji jitihada ya mwili au akili kwa ajili ya kuzalisha mali au huduma. Kufanya kazi ni njia ya kuonesha thamani na utu wa mtu. Wananadharia ya Onomastika kupitia mkabala wa Onomastikifasihi wanaeleza kuwa, majina yanayotumiwa katika kazi za fasihi yanakuwa na madhumuni maalumu, katika kuthibitisha maelezo hayo, watoa taarifa wa utafiti huu wameeleza kuwa, katika methali isemayo:

"Nguo ya Ijumaa hufuliwa Alhamis"

Neno *Alhamis* na *Ijumaa* ni majina ya siku ambayo yametumiwa na watumiaji wa semi hii kwa ajili ya kushajihisha jamii ishikamane na tabia ya kufanya kazi kila siku na kuepuka uvivu. Mtu anaweza kuamka akiwa hana kitu chochote cha kujikimu lakini atakapojitahidi kufanya kazi anaweza kupata mahitaji yake ya msingi. Kwa hivyo, jamii inawajibu wa kujituma na kufanya bidii katika kutafuta kazi, kwa lengo la kuweza kujikimu kimaisha. Watoa taarifa wameeleza kuwa, semi hii inakusudia kueleza kuwa, mtu anatakiwa kufanya kazi kwa wakati na kuepuka uzembe katika kazi. Watoa taarifa wawili walieleza kuwa, kazi ya leo ifanywe leo na isisubiriwe kesho kwani mtu hajui kesho yake.

4.3.2 Kuhimiza uwajibikaji

Uwajibikaji ni mchakato wa kuhakikisha kuwa, watu binafsi au taasisi wanatimiza matarajio ya wadau kwa ufanisi na kwa uaminifu. Uwajibikaji ni sehemu ya motisha au hamasa ya mafanikio ya jambo lolote. Mtu mwajibikaji huwa na sifa zake bainifu; kutimiza majukumu yake kwa wakati, kuwajibika kwa matokeo ya jukumu alilolisimamia iwapo hakutimiza matakwa ya makubaliano, uadilifu na uaminifu, uwazi katika maelezo, kujitolea na uwezo wa kujisimamia. (Greenleaf, 1977).
Kwa ujumla uwajibikaji ni hali ya mtu au kikundi cha watu kukubali na kutekeleza majukumu ipasavyo na kuwa tayari kuwajibika kwa matokeo ya matendo yao, iwe mazuri au mabaya. Bila shaka utafiti huu unadokeza kuwa uwajibikaji ni msingi wa uongozi bora, mafanikio ya kitaaluma na maendeleo ya jamii. Hata hivyo, haitasahaulika utayari wa kujifunza kutoka kwa wafanya kazi wenzake au watu wa nje ya taasisi yake. Nadharia ya Onomastiki kupitia mkabala wake wa Onomastikifasihi inasisitiza kuwa, majina yanayotumika katika ubunifu wa fasihi yanakuwa na makusudio maalumu, kama kusisitiza jamii zao katika uwajibikaji Angalia methali ifuatayo;

*“**Ali** akipanda, **Ali** atavuna”*

Maelezo ya watoa taarifa yanaeleza kuwa katika methali hii kumetumika jina **Ali** kwa kusudio la kuiwakilisha jamii ya watu wanaowajibika katika shughuli zao za kujipatia kipato kwa ajili ya kuendesha maisha yao ya kila siku. Kwa hivyo, jamii nayo haina budi kujenga utamaduni wa kuwajibika katika utekelezaji wa majukumu ili kujikomboa kiuchumi. Aidha, watoa taarifa wameeleza kuwa, ukosefu wa uadilifu hupelekea unyonge kwa baadhi ya watu wasiotendewa haki au uadilifu kwa kutumia msemo huu wa “Aso mtu ana Mungu’’ wamesisitiza kwa kusema kuwa kila mmoja anapaswa kuwajibika kwa nafasi yake.

5.0 Hitimisho

Makala hii imejadili dhima za majina ya pekee katika semi za Kiswahili za Zanzibar. Semi zilizochunguzwa ni methali na misemo. Baada ya utangulizi makala ilifafanua dhana za msingi zilizomo katika makala hii. Badaaye methodolojia na nadharia iliyoongoza utafiti uliozalisha makala hii zilielezwa. Hatimaye mjadala wa matokeo ya utafiti ulifuata, ambapo dhima mbalimbali za majina ya pekee katika methali na misemo zilijadiliwa. Dhima hizo ziligawanywa katika makundi matatu makuu; dhima za kijamii, kiitikadi na kiuchumi.
Kwa ujumla makala hii imetoa mchango mkubwa katika taaluma ya isimu na fasihi ya Kiswahili. Makala inaonesha uhusiano uliopo baina ya vipengele vya lughawiya (majina ya pekee) na tanzu za fasihi (methali na misemo) katika lugha ya Kiswahili. Makala inaonesha nguvu ya uhusiano baina ya lugha na fasihi kama vipengele vya utamaduni wa jamii yoyote ile.
Makala hii inashauri kufanyika kwa tafiti nyengine mbalimbali zenye mwelekeo huu wa kuchambua uhusiano baina ya vipengele vya isimu na vipengele vya fasihi. Eneo hili bado lina pengo kubwa linalohitaji kuzibwa.

Marejeleo

Al-zumar, A. Q. G. (2009). Social Cultural and Linguistic Analysis of Yemeni Arabic Personal Names. GEMA Yemen.
BAKIZA, (2010). Kamusi la Kiswahili Fasaha. Nairobi Kenya. Oxford University Press.
Blanar, V. (2009). Proper Names in the Light of Theorestical Onomastic. Matica Slovenska. Matica.

Bryson, J. M. (2004). What to Do when Steholers Matter. Public Management Rivew.

Crystal, D. (1987). The CambridgeEncyclopedia of Languehe. Cambridbe University Press.

Durkheim, E. (1912). The Elimentary Farm of the Religions Life. Geoge Allen & Anwin Publishers.

Ghassan, M. (2003). Utani Miongoni mwa Waswahili wa Zanzibar. Tanzania Publishing House.

Greenleaf, R. K. (1977). Severty Leadership Jaurney into tha Nature of Legitmet Power and Greatness. Paulist Press.

Liddell, H. G, & Scott, R. (1843). Leddill and Scott's Greek – English Lexicon. Oxford University Press.

Mbele, J. L. (1986). The Liongo Fumo Epic and the schlars Kiswahili. Mnenuka, A. Mtemba, T. Mchepange, S. O. Mosha, E. S. Momanyi, C. Nngungi, P. M. Y. Sosoo, F. K. & Ochieng, D. (WH). (uk: 128 – 145). Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mlaga. W. K (2017). Misingi yaUfundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Karne ya 21. Heko Publishers Ltd.

Mulokozi, M. M. (2017). Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za FasihiVyuo na Vyuo Vikuu. M. M. Mulokozi.

Muslim, M. A. (1950). Al – Maarif. Dar – AL Kutub - lliyya

Njogu. K. & Chimerah, R. (1999). Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu: Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Okal, B. O. (2012) Nafasi ya Tafsiri katika Taaluma ya Onomastiki. Universitu of Dar es salam. Dar es salam Tanzania.

Okpewho, I. (1992). African Oral Litreture Bacgraund, Character nad Continuity. Indina University Press.

Oyaro, CR. (2019). Tafsiri za Methali na Misemo katika Mshale wa Mungu.Tasnifu ya shahada za Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Robbins, L.CH. (1932). An Essay on the Nature and Significance of Economic Science. Macmollon & Co Limited.

Synder, C. R. (1991). The Will and the Ways: Development and and validation of an Individual-defferences measure of hope. APA.

Sasaki, Sh. S. (2006) Chinese Fables: The dragon Skayer and Other Timeless Tales fo Wisdom. Tuttle Publishing.

Trigger, B. G. (1972). Ditermination of Urban Grouth in Pre-industrial Sociaty. Gerald Ducwoth CCompany.

TUKI. (1988) Kamusi ya kiswahili sanifu. Oxford University Press.

TUKI, (2015). English Swahili DDictionary. Dar es Salaam. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu ch Dar es Salaam.

TUKI. (2007). Mithali na Mifano ya Kiswahili. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dare es salaam.

Wa Wamwere, K. (2008). Towards Genocide in Kenya: The curse of negative Ethnicity. Nairobi Mvule Africa Publishers.

www.alhiaya.com.